SIMIYU CO-OPERATIVE UNION (2018) LTD
**CHAMA KIKUU CHA USHIRIKA SIMIYU (2018) LTD**
**SIMCU (2018) LTD**
**Nambari ya Usajili 5603**

**Anuani ya Simu**
**Simu: 0756 065 455**
**Telefax:**
**Barua Pepe: simcu2018ltd@gmail.com**

**Mtaa wa Malambo**
**S.L.P 252**
**Bariadi-SIMIYU**

Unapojibu taja:
**Kumb. Na. AC.105/232/5**

**02/11/2020**

# TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Chama Kikuu cha Ushirika cha Mkoa wa Simiyu [SIMCU (2018) LTD kilichosajiliwa mwezi Juni mwaka 2018 kinachojishughulisha na uzalishaji wa zao la pamba na mazao mchanganyiko kinayo furaha kuwatangazia Watanzania wenye sifa kuomba nafasi ya kazi kwa ajili ya kujaza nafasi wazi kwenye chama hicho.

## 1. MENEJA MKUU (NAFASI 1)

**<u>Sifa za Muombaji</u>:**

(i) Awe amehitimu elimu ya Kidato cha IV/VI na kujiendeleza katika fani za kitaluma na kutunukiwa **Stashahada ya Juu ya Uzamili au Shahada** kutoka katika chuo kinachotambuliwa na Serikali yenye mwelekeo wa; Utawala na Biashara, Uhasibu na Fedha, Menejimenti ya Ushirika (Waliobobea kwenye Uhasibu, Uchumi, Uchumi na Kilimo au Kilimo Biashara.

(ii) Awe na Uzoefu wa kazi usiopungua miaka 3 katika ngazi ya Afisa Mwandamizi kwenye sekta inayojishughulisha na masuala ya ushirika.

**<u>Majukumu ya kazi</u>:**

i. Kuwa Mtendaji Mkuu wa shughuli za kila siku za Chama Kikuu cha Ushirika Simiyu
ii. Kuandaa bajeti ya mwaka na mpango mkakati wa kibiashara kwa kushirikiana na wajumbe wa Bodi ya Chama Kikuu cha Ushirika Simiyu.
iii. Kuwa mtekelezaji wa sera na mipango ya chama kikuu cha ushirika simiyu.

iv. Kuhakikisha taarifa za mapato na matumizi ya chama Kikuu cha ushirika Simiyu zinaandaliwa vyema.
v. Kusimamia ufunguaji na uendeshaji wa akaunti za chama kikuu cha

Ushirika Simiyu.

vi. Kutekeleza na kuzingatia Sera ya Maendeleo ya Ushirika na Sheria nyingine za nchi.
vii. Kutoa ushauri wa kitaalamu kwa Bodi ya Chama Kikuu cha Ushirika Simiyu.
viii. Kuwa Katibu wa mikutano ya Bodi ya Chama Kikuu cha Ushirka Simiyu.
ix. Kushughulikia masuala ya kinidhamu ya watumishi
x. Kuandaa vikao vya Bodi na kamati za Bodi ya Chama Kikuu cha Ushirika Simiyu.
xi. Kuwa mfumbuzi na msuluhishi wa changamoto zinazowakabili wakulima wa pamba na mazao mchanganyiko
xii. Kushirikiana na wadau wengine wa maendeleo katika kutafuta maendeleo ya cha kikuu cha ushirka simiyu.
xiii. Pamoja na majukumu mengine kadri atakavyoagizwa na mamlaka za juu.

**NGAZI YA MSHAHARA**:

Meneja Mkuu ataanza na mshahara wa SIMCUSS – E1 na mshahara unaweza kuongezwa kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na Taratibu za SIMCUSS kulingana na uzalishaji.

**MASHARTI YA JUMLA YA WAOMBAJI**

(i) Wawe na Ujuzi wa kutumia kompyuta
(ii) Wawe na umri usiozidi miaka 45
(iii) Waombaji wote watume picha mbili za passport size za hivi karibuni.
(iv) Waambatanishe Taarifa zao Binafsi (CV)
(v) Waambatanishe Vyeti vya Kuzaliwa
(vi) Waombaji wote waambatanishe nakala ya vyeti halisi vya kuhitimu Elimu ya Sekondari na vyeti vya taaluma
(vii) Waombaji waliosoma nje ya nchi elimu ya Kidato cha IV na VI waambatishe uthibitisho wa vyeti vyao kutoka Baraza la Mitihani Tanzania (NECTA)
(viii) Waombaji waliosoma vyuo nje ya nchi waambatanishe uthibitisho wa taaluma zao kutoka TCU
(ix) Waombaji watakaokidhi vigezo ndio watakaoitwa kwa ajili ya usaili
(x) Maombi yaliyokidhi vigezo vilivyoainishwa ndio watakaoitwa kwenye usaili.
(xi) Waombaji waandike nafasi ya kazi aliyoomba juu ya bahasha

Maombi yatumwe kupitia anuani ya posta kama ifuatavyo:

Kaimu Meneja Mkuu
Chama Kikuu cha Ushirika Simiyu
S. L. P 252
**BARIADI**

**Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 15/11/2020 saa 9:30 alasiri.**

**Limetolewa na:**

EMMANUEL M. MWELELE
**MAKAMU MWENYEKITI**
**CHAMA KIKUU CHA USHIRIKA**
**SIMIYU (2018) LTD**

SIMIYU CO-OPERATIVE UNION (2018) LTD
(SIMCU)
02 NOV 2020
(2018) LTD
S. L. P 252, BARIADI- SIMIYU